# SHANI YA NANJALA NA OTIENO

## Kugundua Upinzani wa Kiuwavijasumu




KWENYE KIJIJI KITULIVU, WANAISHI WATOTO WAWILI, NANJALA NA OTIENO, AMBAO WANAPENDANA SANA. WANAISHI NA MAMA YAO, ASHA, NA BABA YAO, JUMA ...
HAPA, SHIKA!
HEBU TUSHINDANE MBIO!
WATOTO! TAFADHALI INGIENI NYUMBANI ...
OOH! SIJISIKII VIZURI ... NINAJIHISI MDHAIFU


MAMA!
AMEKUWA MGONJWA KWA WIKI MOJA SASA! INAKUA MBAYA ZAIDI!
HEBU TUMPELEKE KITANDANI.
TUTAFANYA NINI?
TUTAKUANGALIA MAMA, TUNAAHIDI!
ASANTENI WATOTO.
WATOTO WANA WASIWASI KUHUSU MAMA YAO! UNADHANI NI NINI KITAKACHOFANYIKA? HEBU TUANGALIE VIZURI NDANI YA MWILI WAKE ILI TUJUE...



NDANI YA MWILI WAKE, MAMA YAO, ASHA, ANAPIGANA VITA!
TUMEVAMIWA!
TUNACHUKUA NAFASI, HIVI KARIBUNI TUTAMSHINDA HUYU MWANADAMU DHAIFU!
TUNAPASWA KUSAIDIA KUMLINDA MAMA DHIDI YA WAVAMIZI HAWA!
MIMI NDIYE KIONGOZI WA ASKARI WAZURI AMBAO WANASAIDIA KUMUOKOA MAMA WA WATOTO. SISI TUMEVAMIWA NA WAVAMIZI WANAOITWA BAKTERIA WAMEMFANYA MAMA AWE MGONJWA SANA.
TUNAFANYA KAZI NZURI LAKINI NADHANI TUNAHITAJI MSAADA!
NAKUBALI! KWA KWELI, KWA SABABU NI BAKTERIA ZINAZAMFANYA MAMA AWE MGONJWA, ANAHITAJI AINA MAALUM YA DAWA INAYOITWA VIUWAVIJASUMU ILI KUMSAIDIA KUPATA HALI BORA.
VIUWAVIJASUMU NI MADAWA YA KUSHANGAZA KWA SABABU WANAWEZA KUPIGANA DHIDI YA BAKTERIA!
NATUMAI WATOTO WAKE WEREVU WATAWEZA KUMSAIDIA, WATAENDA KWENYE SHANI KUMUOKOA MAMA YAO!
NITAFUATILIA NIKIELEZEA KILE KINACHOTOKEA NA TUNAWEZA KUJIFUNZA KWA PAMOJA NI JINSI GANI TUNAWEZA KUMUOKOA MAMA...


WAKATI HUO HUO, NJE YA MWILI, MAMA ANA WAZO KUHUSU NI NINI KINAWEZA KUMSAIDIA KUPATA NAFUU...
WATOTO, TAFADHALI MUNAWEZA KUNILETEA SANDUKU LA MADAWA KUTOKA KWENYE RAFU?
HIZI NI NINI? JE, ZITAMFANYA APATE NAFUU?
SIJUI, LAKINI NADHANI NILIMWONA BABA AKIKUNYWA BAADHI YAZO MUDA MREFU ULIOPITA. LABDA ZITAMSAIDIA PIA?
ANGALIA, MAMA ANAKUNYWA DAWA ZILIZOWEKWA KWA NYUMBA TANGU WAKATI WA MWISHO MTU ALIPOKUWA MGONJWA ...
JE! UNADHANI ZITAMSAIDIA MAMA KUPATA NAFUU? HEBU TUANGALIE NDANI YA MWILI WAKE TENA KWENYE UKURASA UFUATAO ILI TUBAINI ...


NDANI YA MWILI WA MAMA ...
SISI NI WAZEE SANA KUPIGANA DHIDI YA BAKTERIA HIZI ...
OH HAPANA! INAONEKANA KAMA BAKTERIA ZITAZISHINDA DAWA!
TUNAWEZA KUZISHINDA KWA URAHISI!
KUZISHINDA HIZI DAWA ZA ZAMANI, ZILIZOISHA NGUVU KUNATUFANYA KUWA NA NGUVU ZAIDI!
EXPIRY DATE 2016
UNAKUMBUKA WAKATI MAMA ALIKUNYWA DAWA HIZO? ALISAHAU KUANGALIA TAREHE KWENYE KISANDUKU NA INAONYESHA KUWA DAWA HIZI NI ZA ZAMANI NA HAZIFANYI KAZI TENA.
KUNYWA MADAWA HAYO YA ZAMANI KWA KWELI KUMEZISAIDIA BAKTERIA KUWA NA NGUVU ZAIDI!


INAONEKANA DAWA NILIZOZITUMIA HAZIJAFANYA KAZI, NANAHISI VIBAYA ZAIDI SASA ...
TUNAWEZA KUFANYA NINI KUMSAIDIA MAMA?
TAFADHALI UNAWEZA KWENDA KWA DUKA KUPATA DAWA TOFAUTI?


NJOO OTIENO, HEBU TUENDE TUTAFUTE DAWA TOFAUTI ZITAKAZOMSAIDIA MAMA KUPATA NAFUU!
NANJALA NA OTIENO WANAANZA KUTEMBEA KWENDA KWENYE MJI WA KARIBU AMBAKO KUNA DUKA LA KUUZA MADAWA ...
WATOTO WANAENDA ILI WAMSAIDIE MAMA YAO, HEBU TUENDE NAO TUONE KILE WANACHOKIPATA NJIANI!



WATOTO WANAMPITA JIRANI YAO AMBAYE ANALISHA NG'OMBE WAKE ...
OH ANGALIA, BWANA WAFULA YUKO NA NG'OMBE WAKE.
NDIYO, NASHANGAA ANAFANYA NINI?
HABARI WATOTO, NG'OMBE WANGU WENGINE NIWAGONJWA. NIMEKUWA NIKIWADUNGA SINDANO ILI WAPONE, LAKINI HAIONEKANI KAMA INAFANYA KAZI!
NATUMAINI ITASAIDIA KWA SABABU ENDAPO NG'OMBE ZANGU ZITAKUFA NITATUNZAJE FAMILIA YANGU?
MASKINI BWANA WAFULA, NATUMAI NG'OMBE ZAKE WATAPATA NAFUU.
NDIO, MIMI PIA! NASHANGAA NI KWA NINI DAWA HAIZISAIDII ...
NI KAMA KINACHOMFANYIKIA MAMA! KUNA KITU LAZIMA KINAENDELEA ...
WATOTO HAWA NI WEREVU SANA! WAMEGUNDUA KUWA DAWA AMBAYO BWANA WAFULA ANAWAPA NG'OMBE ZAKE HAIFANYI KAZI ILI KUWAFANYA KUWA NA NAFUU NA NI KAMA TU KINACHOMFANYIKIA MAMA YAO.
NADHANI TUNAPASWA KUJIFUNZA ZAIDI KUHUSU JINSI MADAWA HUTUMIWA KWA WANYAMA ILI KUJARIBU KUFANYA KITU KINACHOENDELEA! NJOO PAMOJA NAMI NA TUTAENDA NA KUTAFUTA MAJIBU ...


MBELE KIDOGO, WATOTO WANAKUTANA NA MMOJA WA WAZEE WA KIJIJI ALIYEKUWA ANAELEKEA SOKONI ...
HABARI WATOTO, MUNAKWENDA WAPI? MNAONEKANA MKO NA WASIWASI.
TUNAENDA KUNUNUA DAWA YA MAMA YETU AMBAYE NI MGONJWA.
TAYARI TULISHAMPA DAWA ZINGINE NYUMBANI LAKINI HAZIKUFANYA KAZI.
KISHA TULIMWONA BW WAFULA NA ANA SHIDA SAWA KWA NG'OMBE ZAKE. HATUJUI KINACHOENDELEA!
SIJUI NI NINI KINACHOSABABISHA TATIZO HILI, LAKINI NAJUA KUWA NI MUHIMU KUYATUMIA MADAWA KWA MAKINI NA KUYATUMIA VIZURI.
NINAHAKIKISHA KUWA NINATUMIA MADAWA KWAWANYAMA WANGU WAKATI WANAPOKUWA WAGONJWA TU. WATU WENGINE WANAWEZA KUWAPA ILI KUWAFANYA WANYAMA KUKUA KWA HARAKA, ILA HILI SI WAZO NZURI.
HII NI SAWA KABISA! KUWAPA DAWA HIZO MAALUM ZINAZOITWA VIUWAVIJASUMU WAKATI WANYAMA SI WAGONJWA, ZINAWEZA SABABISHA DAWA KUTOFANYA KAZI VIZURI.
HII NI KWA SABABU BAKTERIA ZINAWEZA KUWA NA NGUVU ZAIDI KILA WAKATI WANAPIGANA NA DAWA NDANI YA MWILI!
ENDAPO BAKTERIA ZITAKUWA NA NGUVU SANA BASI WAKATI WANYAMA WANAPOKUWA WAGONJWA, VIUWAVIJASUMU HAVIWEZI KUWAFANYA KUPATA NAFUU! KUNA JINA MAALUM KWA HILI. INAITWA UPINZANI WA KIUWAVIJASUMU
JE! UNAFIKIRI HII NDIYO INAWEZA KUWA IMEIFANYIKIA DAWA YA BW WAFULA ANAYOTUMIA KUJARIBU KUSAIDIA NG'OMBE WAKE?
10


WAKATI NINAPOHITAJI KUTUMIA VIUWAVIJASUMU KWA WANYAMA WANGU, MIMI SINYWI MAZIWA KUTOKA KWA WANYAMA HAO. NEMBO KWENYE CHUPA INASEMA KWAMBA UNAPASWA KUSUBIRI MUDA FULANI KABLA YA KUNYWA MAZIWA HAYA TENA. NADHANI NI BORA KUFANYA HIVYO.
NI SAWA NA KUUZA WANYAMA KWA NYAMA. SIUZI WAGONJWA AMBAO WAMEKUWA WAKITUMIA VIUWAVIJASUMU SILI WANYAMA HAWA MWENYEWE AU KUPEANA NYAMA KWA FAMILIA YANGU PIA.
JUU YA CHUPA YA DAWA INAKWAMBIA NI MUDA GANI UNAPASWA KUSUBIRI KABLA YA KULA NYAMA TENA NA NADHANI NI BORA KUSUBIRI HADI WAKATI HUU UMEKWISHA.
HII NI KWELI KABISA! NI VYEMA KUTOKUNYWA MAZIWA AU KULA NYAMA KUTOKA KWA WANYAMA WANAOTIBIWA NA VIUWAVIJASUMU KWA SABABU DAWA INAWEZA KUINGIA NYAMA NA MAZIWA.
Viuwavijasumu
IKIWA UNAKULA AU KUNYWA HAYA, VIUWAVIJASUMU VINAWEZA KUINGIA KATIKA MWILI WAKO NA KUSABABISHA BAKTERIA KUWA NA NGUVU ZAIDI, KUONGEZA UPINZANI VIUWAVIJASUMU. UNAWEZA KUANGALIA CHUPA YA DAWA ILI KUJUA JINSI YA KUTUMIA VIZURI NA KWA USALAMA. ITAKUAMBIA SIKU NGAPI KUSUBIRI KABLA YA KUNYWA MAZIWA NA KULA NYAMA TENA.
ASANTE SANA KWA KUTUAMBIA MAELEZO HAYA YOTE MUHIMU. TANGU SASA TUTAANGALIA CHUPA YA DAWA!


WATOTO BADO WANAKWENDA MJINI KUNUNUA DAWA TOFAUTI YA MAMA YAO...
TAZAMA HAYA MABOMBA YOTE!
YANATOKA WAPI?
SIJUI, OTIENO. LAKINI JE, UNADHANI KUNA UHUSIANO KATI YA MABOMBA HAYA NA UGONJWA WA MAMA?
Hospitali
Kiwanda cha dawa
Maji taka
WATOTO HAWA NI WEREVU SANA! WAMEONA KITU KINGINE MUHIMU SANA! HEBU TUANGALIE KWA UKARIBU...
TAKA ZITOKAZO HOSPITALI, MAJI TAKA NA VIWANDA VITENGENEZVYO VIUWAJISUMU ZINAWEZAKUINGIA KWENYE MITO NA KUCHAFUA MAZINGIRA. HII NI NJIA MOJAWAPO INAYOWEZA KUSABABISHA UPINZANI WA VIUWAJISUMU!
JE, UNAKUMBUKA TULIPOJIFUNZA KUHUSU HILI AWALI? NI WAKATI MADAWA MAALUM HAYAWEZI KUPIGANA TENA NA BAKTERIA KWA SABABU ZIMEZIZOEA SANA NA BAKTERIA ZINA NGUVU SANA!


TAZAMA NANJALA,
ZILE NI DAWA ZAELEA
KWENYE MTO?
DAWA
Viuwavijasumu
ANGALIA HAPA!
TATIZO SI KUYATUMIA SANA TU,
PIA KUTOYATUPA MBALI VIZURI! DAIMA NI
SALAMA KURUDISHA DAWA ZISIZOTUMIWA
NA CHUPA TUPU KWA DAKTARI AU DUKA LA
DAWA.


WATOTO HATIMAYE WAMEFIKA MJINI ...
ANGALIA OTIENO ... NDIO LILE DUKA AMBALOTUNAWEZA KUNUNUA DAWA!
DUKA LA DAWA
AGR
HABARI, TUNAHITAJI DAWA YA MAMA YETU YEYE NI MGONJWA SANA! TAFADHALI UNAWEZA KUTUSAIDIA?
HAPA, JARIBU VIDONGE HIVI.
NANJALA, MTU HUYO ANAJUAJE NI DAWA ZIPIZITAFANYA KAZI NA NI VIDONGE VINGAPI AMBAVYO MAMA YETU ANAHITAJI?
SINA UHAKIKA OTIENO ... SIJUI NI JINSI GANI ANAWEZA KUJUA MAMA AKO NA SHIDA GANI ILHALI HAJAMWONA...
JE! ZITAMFANYA APATE NAFUU?
KUNA NJIA MOJA TU YA KUJUA!
BAADA YA KILA KITU TUMEJIFUNZA, UNADHANI DAWA HII ITAMSAIDIA MAMA? HEBU TUONE KINACHOTOKEA BAADAYE ...


WATOTO WAMEFIKA NYUMBANI NA KUPATA MAMA YAO AMEZIDIWA ZAIDI ...
MAMA!
HAPA, TUMEPATA DAWA TOFAUTI ... TAFADHALI KUNYWA HIZI!
TUTAJUAJE KAMA INAFANYA KAZI?
NATUMAI ATAANZA KUONEKANA MWENYE NAFUU HIVI KARIBUNI!
JE, UNADHANI DAWA AMBAZO WATOTO WALINUNUA KUTOKA DUKANI ZITASAIDIA? HEBU TUANGALIE TUJUE ...



NDANI YA MWILI WA MAMA, MAPAMBANO YANAENDELEA KUWA MAKALI ZAIDI...
BAKTERIA HIZI ZINA NGUVU MNO! HATUWEZI KUZISHINDA!
TUNASHINDA! HAKUNA KITU UNAWEZA KUFANYA KUHUSU HILO!
JE! HII INATOKEAJE? TUNAPAMBANA KADRI YA UWEZO WETU LAKINI ZINATUSHINDA!
OH HAPANA!
INAONEKANA NI KAMA MADAWA HAYA MAPYA HAYATAFANYA KAZI! NI KWA SABABU BAKTERIA HIZI NI SUGU KWA VIUWAVIJASUMU AMBAVYO WATOTO WAMENUNUA!
MTU ALIYEKUWA AKIUZA DAWA KATIKA DUKA HAKUJUA NI AINA GANI YA BAKTERIA ILIYOFANYA MAMA AWE MGONJWA NA NI VIUWAVIJASUMU GANI VILIVYOPASWA KUZIUA! HAKUJUA KWAMBA BAKTERIA HIZI NI SUGU!
JE! UNAWEZA KUKUMBUKA BAADHI YA MAMBO TULIYOYAPATA AMBAYO HUSABABISHA UPINZANI?
KUCHUKUA DAWA AMBAYO NI YA ZAMANI.
EXPIRY DATE 2016
KUNYWA MAZIWA KUTOKA KWA WANYAMA WALIOTIBIWA NA VIUWAVIJASUMU.
KUTUPA VIUWAVIJASUMU KWENYE MAZINGIRA.
KUINGIA KWA TAKA CHAFU KENYE VIINGIZI VYA MAJI.
MAZIWA


WAKATI HUO HUO, WATOTO WAMEGUNDUA KUWA DAWA HAZIMSAIDII MAMA YAO...
VIDONGE HAVIKUMSAIDIA, ANAZIDI KUWA VIBAYA ZAIDI ... TUNAPASWA KUFANYA KITU!
NADHANI ANAHITAJI KUMUONA DAKTARI. MTU ALIYE KWENYE DUKA LA DAWA HAKUWEZA KUTUSAIDIA LAKINI DAKTARI ATAKUWA NA MAFUNZO MAALUM YA KUJUA NI NINI HASA KINASUMBUA!
WAZO NZURI! BW WAFULA ANA PIKIPIKI, LABDA ANAWEZA KUMPELEKA?
MAMA YETU BADO NI MGONJWA NA ANAENDELEA KUDHOOFIKA ZAIDI. TUNAFIKIRIA ANAHITAJI KUMUONA DAKTARI. TAFADHALI UNAWEZA KUMBEBA KWENYE PIKIPIKI YAKO?
NDIO, BILA SHAKA WATOTO. KWA NINI MSIJE PIA?
NDUGU YANGU PIA ANA PIKIPIKI... NITAMWITA NA TUNAWEZA KWENDA PAMOJA. MAMA YAKO ANAWEZA KUWAHITAJI!
WATOTO WANAMPELEKA MAMA YAO KWENYE KITUO CHA AFYA... WAO WANAAMINI KWAMBA DAKTARI ANAWEZA KUSAIDIA!


HOSPITAL
DAKTARI ANAFANYA BIDII ILI KUFAHAMU NI NINI KIBAYA NA MAMA ...
HONGERA WATOTO! MMEFANYA VIZURI SANA KUMLETA MAMA YENU KUNIONA, YEYE NI MGONJWA SANA!
TULIJARIBU KUMSAIDIA KWA KUMPA DAWA NYUMBANI ...
NAJUA, LAKINI HILI HALINGEWEZA KUMSAIDIA KWA SABABU BAKTERIA WANAOMFANYA MGONJWA NI SUGU KWA BAADHI YA VIUWAVIJASUMU.
KISANDUKU CHA KUPIMA DAMU
NI SUGU? JE! HILO LINAMAANISHA NINI?
WACHA NIWAELEZEE...
VIUWAVIJASUMU NI MADAWA MAALUM SANA, ILAKILA WAKATI TUNAPO VITUMIA KUTIBU WATU NA WANYAMA, BAKTERIA ZISABABISHAZO UGONJWA HUO HUWA NA NAFASI YA KUJIFUNZA JINSI YA KUPAMBANA NA DAWA HIZI. JINSI BAKTERIA ZINAKUWA NA NGUVU ZAIDI, VIUWAVIJASUMU HAVIFANYI KAZI VIZURI TENA.
IKIWA VIUWAVIJASUMU VYOTE VITAACHA KUFANYA KAZI, HATUWEZI KUWAFANYA WATU WAPONE WAKATI WATAKAPOGONJWEKA KUTOKANA NA BAKTERIA, NA HII ITAKUWA MBAYA SANA! NDIO MAANA NI MUHIMU SANA KWAMBA SISI WOTE TUTUMIE VIUWAVIJASUMU KWA MAKINI SANA.
HII INA MAANA KUWA NI LAZIMA TUZITUMIE TU WAKATI SISI AU WANYAMA WETU NI WAGONJWA SANA NA TUNAPASWA KUHAKIKISHA TUNATUMIA AINA SAHIHI ZA VIUWAVIJASUMU KWA KUZUNGUMZA NA DAKTARI AU DAKTARI WA WANYAMA. KISHA VIUWAVIJASUMU VITAENDELEA KUFANYA KAZI KWA MUDA MREFU NA WATU WATAWEZA KUPATA NAFUU TENA!
NI VIZURI SANA! NINA FURAHA SANA DAKTARI ANAWEZA KUWAAMBIA WATOTO KINACHOFANYIKA!


DAKTARI AMETAMBUA KILE KINACHOENDELEA! SASA ANAWEZA KUSAIDIA KUFANYA MAMA BORA...
NIMETAMBUA NI BAKTERIA ZIPI ZINAZOKUFANYA UKUWE MGONJWA NA NI VIUWAVIJASUMU VIPI VITAKAVYOFANYA KAZI ILI UPONE.
VIDONGE HIVI VINAPASWA KUMEZWA NA WEWE TU, SIO MTU MWINGINE YEYOTE, KWA SABABU NI MAALUM KWA BAKTERIA ZINAZOKUFANYA MGONJWA.
TAFADHALI MEZA VIDONGE VYOTE NINAVYOKUPA, NI MUHIMU KUFANYA HIVYO ILI BAKTERIA ZOTE NI ZIWEZE KUUAWA NA VIUWAVIJASUMU NA ZISIWEZI KUKURUDIA NA KUKUFANYA MGONJWA TENA.
HAKUPASWI KUSALIA YOYOTE, LAKINI IKIWA KUNA VIUWAVIJASUMU VYOVYOTE VYA ZAMANI ULIVYOVIACHA NYUMBANI TAFADHALI VILETE HAPA KWENYE KLINIKI NA TUNAWEZA KUVITUPA KWA NJIA IFAAYO.
NI SAWA KUWEKA NYUMBANI DAWA ZA KAWAIDA KUTOKA KWA DUKA LA DAWA, KAMA VILE VIDONGE VYA KUONDOA MAUMIVU YA KICHWA, LAKINI DAWA MAALUM KAMA VIUWAVIJASUMU AMBAVYO HUPATIKANA KWA DAKTARI LAZIMA VISITUMIWE BILA KUPATA MAAGIZO KUTOKA KWETU KWANZA. IKIWA HUJUI IPI NDIO IPI, UNAWEZA KUTUULIZA.
ASANTE DAKTARI, NADHANI DAWA HII TAYARI INASAIDIA!
WATOTO WAKO NI WEREVU SANA!
WALIGUNDUA KUNA KITU HAKIKO SAWA WAKATI DAWA HAZIKUFANYA KAZI NA KUKULETA UNIONE KWA WAKATI!
NAJUA ... NINAJIVUNIA SANA. ASANTE WATOTO.


WAKATI HUO HUO, NDANI YA MWILI WAKE, VIUWAVIJASUMU DAKTARI ALIVYOMPA MAMA VINAFANYA KAZI...
TUNASHINDA!
OH HAPANA ... WANATUSHINDA!
TUTAWEZA KUZISHINDA BAKTERIA HIZI MBAYA!
WATOTO WALIFANYA JAMBO ZURI KUMPELEKA MAMA YAO KWA DAKTARI. ANGALIA! VIUWAVIJASUMU ALIVYOPEWA TAYARI VINAFANYA KAZI ILI KUZUIA BAKTERIA!


SIKU MBILI BAADAYE... MAMA ANAHISI VIZURI ZAIDI! KUNA MSHANGAO MKUBWA KWA WOTE...
BABA!
HABARI WATOTO! MUMEKUWA VIZURI?
ILIBIDI TUMCHUNGE MAMA ... YEYE HAKUWA ANAHISI VIZURI NA ALIHITAJI KUTIBIWA NA DAKTARI!
WATOTO WALINISAIDIA KUPATA NAFUU, WALIKUWA SHUJAA SANA NA WALIPATA MSAADA WAKATI NILIUHITAJI.
NILIKUWA MGONJWA KWA SABABU YA BAKTERIA SUGU!
HIYO NI NINI?
TUNAWEZA KUKUAMBIA YOTE KUHUSU HILO!
BAADAYE, BAADA YA WATOTO KUMWAAMBIA BABA YAO KILA KITU WALICHOJIFUNZA ...
ASANTE KWA KUNIAMBIA KUHUSU HILI. INAONEKANA NI SUALA MUHIMU NA NADHANI TUNAHITAJI KUMUELEZA HABARI HII KILA MTU. NITAITA MKUTANO WA JUMUIYA.


KATIKA MKUTANO WA JUMUIYA, KILA MTU AMEJIFUNZA KUHUSU UPINZANI WA VIUWAVIJASUMU NA NINI WANAWEZA KUFANYA ILI KUACHA KUWA MBAYA ZAIDI ...
ASANTENI NYOTE KWA KUJA, TUTAJADILI SUALA MUHIMU SANA. NIMEMWAALIKA DAKTARI NA DAKTARI WA WANYAMA HAPA NA PIA KUHAKIKISHA SISI WOTE TUNAELEWA HASA KILE TUNACHOPASWA KUFANYA ...
NI LA KUSISIMUA SANA HIVO KWAMBA TUMERUHUSIWA KUJA KWA MKUTANO!
NAJUA! BABA ALISEMA NI RUHUSA MAALUM KWA SABABU TULIKUWA WA MANUFAA SANA KUJUA NI NINI KILICHOMSUMBUA MAMA NA KUMSAIDIA KUPATA NAFUU!
KILA MTU ANA HAMU SANA KUJIFUNZA KUHUSU UPINZANI WA VIUWAVIJASUMU NA NI NINI WANAWEZA KUFANYA KUHUSU HILO! KUNA MASWALI MENGI ...
JE! UNAWEZA KUNISAIDIA KUJUA NI KIUWAVIJASUMU KIPI AMBACHO NINAFAA KUTUMIA KWA NG'OMBE WANGU? BADO HAWAJAPATA NAFUU NA DAWA NILIYOKUWA NAYO. NINA WASIWASI WAO WANA BAKTERIA SUGU!
NDIYO, BILA SHAKA! NINAWEZA KUSAIDIA KUJUA UGONJWA WANAOUGUA NA JINSI TUNAPASWA KUUTIBU. NAWEZA PIA KUWACHANJA WANYAMA WAKO DHIDI YA MAGONJWA MENGINE HIVYO KUPUNGUZA UWEZEKANO WA KUW WAGONJWA SIKU ZA USONI!
NI MUHIMU KUMRUHUSU TU DAKTARI WA WANYAMA MWENYE UJUZI KUWACHANJA WANYAMA WAKO HIVYO UNAJUA NI CHANJO SAHIHI AMEWAPEA.
MWISHONI MWA MKUTANO, BABA YAO ANA TANGAZO MAALUM LA KUFANYA ...
NINGEPENDA KUSEMA ASANTE KWA WATOTO WANGU, NANJALA NA OTIENO, KWA KUJUA KUHUSU UPINZANI WA VIUWAVIJASUMU NA KUSAIDIA MAMA YAO KUPATA NAFUU. WAO NI WATOTO WENYE UJASIRI SANA NA WEREVU!


SASA UMEJIFUNZA KUHUSU UPINZANI WA VIUWAVIJASUMU PIA, NI MUHIMU KWAMBA MUENEZE UJUZI HUU ILI KILA MTU AJUE KUUHUSU!
KOTE DUNIANI, KILA MTU ANAKABILIWA NA CHANGAMOTO HII NA TUNAPASWA KUFANYA KAZI KWA PAMOJA! KISHA TUNAWEZA KUHAKIKISHA DAWA ZINAENDELEA KUFANYA KAZI NA WATU NA WANYAMA WANAWEZA KUKAA NA AFYA!

